

# Shughuli za kukamilisha nyumbani

## Habari kwa wazazi na walezi

Ili kuimarisha kile anachojifunza shuleni mtoto wako atapokea shughuli ambazo huenda angependa kukamilisha akiwa nyumbani.

Umtie moyo mtoto wako kukamilisha shughuli zile na zungumza naye kuhusu kazi yake. Kumsaidia mtoto wako kwa njia hii hukupa uelewa wa kile anachojifunza shuleni na kumwonyesha kuwa unathamini elimu na kujifunza.

Kukamilisha shughuli akiwa nyumbani itampa mtoto wako fursa ya:

- kurekebisha mambo ambayo amejifunza shuleni,
- kuongeza ufahamu na ustadi wake,
- kukuza ustadi wa kusoma ambao atatumia maisha yake yote.

## Kuanzisha tabia nzuri nyumbani

Kuwa na tabia nzuri kutasaidia mtoto wako katika maisha yake yote ya shule na kazini.

- Weka muda wa kila mara kukamilisha shughuli zile – huu uwe wakati sawa kila siku.
- Chagua muda ambao unafaa zaidi kwa mtoto wako (watoto wengine huzingatia vyema asubuhi, wengine mchana).

Mtoto wako ataona ni rahisi zaidi kuzingatia ikiwa ana nafasi nzuri.

- Weka nafasi tulivu na yenye mwanga wa kutosha ili mtoto wako afanye kazi.
- Weka vitu anavyohitaji karibu kwake kama vile pensili, karatasi au kompyuta.
- Pata mahali pasipo na visumbufu (kwa mfano, mbali na televisheni au michezo ya kompyuta).

## Ninawezaje kumsaidia mtoto wangu?

- Uwe mdadisi na uliza maswali kuhusu anachofanya.
- Umwulize kukufundisha kile anachojifunza.
- Angalia ikiwa anahitaji usaidizi.
- Sifu juhudhi zao anapojaribu na kukamilisha shughuli.
- Uliza mwalimu kupata nyenzo zozote zinazopatikana zinazosaidia wazazi na walezi.

Kumbuka, kukamilisha shughuli akiwa nyumbani kunapaswa kuwa uzoefu mzuri kwa mtoto wako.

Julisha mwalimu ikiwa mtoto wako anahitaji usaidizi wa ziada au marekebisho maalum ili kukamilisha shughuli.

## Huduma ya mkalimani wa simu

Ikiwa unahitaji usaidizi wa mkalimani, tafadhali piga simu 131 450, mwambie opereta ni lugha gani unayohitaji na umwombe apige simu shuleni. Opereta atapata mkalimani kwenye simu kukusaidia na mazungumzo. Hutatozwa kwa huduma hii.